## Maswali

1. Isaka na Rebeka waliita mapaja majina gani?
2. Paja mkubwa alikuwa nani? Alifanya kazi gani alipokuwa mkubwa?
3. Paja mdogo alikuwa nani? Alifanya kazi gani alipokuwa mkubwa?
4. Mungu alisema nani atakuwa na baraka?
5. Mbona Esau aliuza haki yake ya mzaliwa wa kwanza?
6. Isaka alitaka Esau afanye nini kabla ya kumpa baraka?
7. Rebeka alifanya nini?
8. Isaka alidanganywa namna gani?
9. Esau alipanga kufanya nini kwa sababu Yakobo alikuwa amebarikiwa?
10. Yakobo alitumwa kwenda wapi?

## Majibu

1. Esau na Yakobo.
2. Esau alikuwa paja mkubwa. Alikuwa mwindaji.
3. Yakobo alikuwa paja mdogo. Alikuwa mchungaji.
4. Mungu alisema paja mdogo atakuwa na baraka.
5. Esau aliuza haki yake ya mzaliwa wa kwanza kwa sababu alikuwa na njaa na Yakobo alikuwa ametengeneza chakula. Aliuza haki yake ya mzaliwa wa kwanza kwa ajili ya chakula.
6. Isaka alitaka Esau aende awinde swara na amtengenezee chakula.
7. Rebeka alichinja mbuzi, akaweka ngozi yake kwa Yakobo na akamvaa mavazi ya Esau.
8. Isaka akapapasa kwa ngozi ya mbuzi. Akanusia nguo ya Esau. Akajua kwamba Yakobo ni mwanawe Esau.
9. Esau alimchukia Yakobo na akapanga kumuua.
10. Yakobo alitumwa kuenda kuishi Harani kwa mjomba wake.

## SHULE YA JUMAPILI YA CBM

### Awamu ya 1 Mwaka wa 3

# 8 Yakobo na Esau

## Marejeo

Mwanzo mlango 25 : 19 – 34 na mlango wa 27

## Kiini cha somo

Kuonyesha vile uongo na chuki iligawanyisha familia ya Yakobo na kusababisha huzuni mwingi. Kuonyesha kwamba Mungu hutimiza ahadi zake KILA MARA.

## Maneno maalum

8.1 Mapacha + Esau ndiye mkubwa + nyekundu na malaika + Yakobo ndiye mdogo + ngozi laini + Esau mwindaji + Yakobo mchungaji

8.2 Isaka alipenda Esau + Rebeka alipenda Yakobo + Mungu alisema Yakobo atapata baraka

8.3 Esau ana njaa + Yakobo anapika chakula + Esau anauza haki ya mzaliwa wa kwanza + Yakobo atapata ahadi za Mungu.

8.4 Isaka + Esau anaenda kuwinda + tengeneza chakula + Rebeka alipika mbuzi + Yakobo ana ngozi ya mbuzi + mavazi ya Esau.

8.5 Yakobo chakula kwa Isaka + akapapasa ngozi ya mbuzi + alinusia nguo za Esau + alibariki Yakobo

8.6 Esau nyumbani + Yakobo alikuwa na baraka + aliudhika sana

8.7 Esau ana hasira + Yakobo anatoroshwa + Harani + mjomba Labani.

**8.1** Isaka na Rebeka walikuwa na furaha kubwa kwa sababu walikuwa na wana wawili – Yakobo na Esau. Walikuwa mapaja. Esau alikuwa paja mkubwa na Yakobo alikuwa paja mdogo. Hata kama Yakobo na Esau walikuwa mapaja lakini walikuwa tofauti sana. Esau paja mkubwa alikuwa mnene na wa nguvu, tena mwili wake wote ulikuwa na malaika wekundu. Lakini Yakobo alikuwa mpole na ngozi yake nyepesi tena nyororo.



Esau alipokua alikuwa mwindaji. Alikuwa na upendo wa kuwinda swara akikimbizana nao. Wakati alikuwa nje akiwinda, alipenda kuishi kwa vilima na msituni. Yakobo alikuwa mchungaji. Alipenda kutulia nyumbani akichunga kondoo na mifugo wengine.

**8.2** Isaka alipenda Esau saidi kwa maana alimletea nyama aliyopenda. Lakini Rebeka alipenda Yakobo aliyekuwa mpole na mngwana. Kabla mapaja wazaliwe, Mungu alikuwa ameambia Rebeka kwamba atabariki mwana mdogo badala ya mwana mkubwa

**8.3** Siku moja Esau alikuwa ameenda kuwinda. Hakukuwa na chakula kwa siku kadha na akawa na njaa sana. Alipokuja nyumbani alipata Yakobo amepika chakula. Esau aliuliza Yakobo amsaidie hicho chakula. Yakobo alimwambia atamuuzia hicho chakula kwa kununua baraka za haki zake za mzaliwa wa kwanza. Esau aliangalia chakula kilichokuwa kikipigwa mekoni. Alikuwa na njaa sana na hakujali ahadi za Mungu za haki za mzaliwa wa kwanza. Alikubali na akauuzia Yakobo haki zake za kuzaliwa. Alikaa chini na akafurahi akila chakula.

Esau alikuwa ameuza haki yake ya kuzaliwa. Hii ilimaanisha baraka za Isaka na ahadi za Mungu alizoahidi Ibrahimu sasa zilielekezwa kwa Yakobo.

**8.4** Isaka alipokuwa mzee, mgonjwa na hakuweza kuona, aliita Esau. Alimwambia aende kuwinda, alete swara na amtengenezee chakula alichokipenda. Halafu angempea baraka.

Wote wawili hakuna aliyemwona Rebeka akinyemelea polepole akienda nje ya hema. Kwa haraka aliita Yakobo alete mbuzi wawili wachanga kutoka kwa kikundi ili apike. Chakula kilipokuwa kikiiva, alivalisha Yakobo mavazi ya Esau. Kwa umakini, alishonea Yakobo ngozi ya mbuzi kwenye shingo na kwa mikono ili Isaka ahisi kuna malaika kama ya Esau.

Mungu alikuwa amesema kwamba Yakobo atapata baraka, na WAKATI WOTE Mungu hutimiza alilosema. Lakini Rebeka alisahau hiyo. Alitaka kuona kwamba ni yeye alimwezesha Yakobo kubarikiwa. Kwa hivyo alituma Yakobo kudanganya Isaka.

**8.5** Yakobo alipelekea Isaka chakula kwa hema. Baba yake angejuaje kwamba yeye si Esau? Alimwiita, “Babangu.” Isaka aliuluza, “Wewe ni nani?” Yakobo alimjibu, “Mimi ni Esau mwanao mkubwa. Angalia nimeshika swara vile uliniambia. Hebu keti ule chakula na unibariki.”

Isaka alimuuliza, “Ulipata swara haraka namna gani?” Yakobo alijibu, “Bwana alinileteа.” Isaka alishangaa sana. Sauti ilikuwa ya Yakobo. Kwa upole alisema, “Kuja karibu nikushike nione kama kweli wewe ni mwanangu Esau.” Yakobo alisonga mbele. Isaka alishikashika kwa manyoya ya mbuzi iliyokuwa kwa mikono yake.

“Kweli wewe ni Esau.” Isaka alisema, na akala chakula. Yakobo aliposongea karibu ili abarikiwe, Isaka alinusia harufu ya mawindo kwa mavazi ya Isaka yenye Yakobo alikuwa amevaa. Hapo Isaka alijua ni Esau na akambariki.

**8.6** Bunde tu Yakobo aliondoka kwa hema, Esau alifika na chakula ametengenezea babake. Isaka alipohakikisha kwamba yeye ni Esau, aliudhika sana. Aliuliza, “Nimembariki nani?”

Isaka alimwelezea vile Yakobo alikuwa amemletea chakula na amembariki. Esau aliposikia hayo, alilia sana kwa sauti. Alipiga magoti na kulilia babaye ili ambariki naye pia. Lakini baraka zilikuwa zimemwendea Yakobo zamani. Esau hangeweza kupata zingine.

**8.7** Esau aliona vibaya na kukasirika sana kwa sababu Yakobo alikuwa amebarikiwa badala yake. Alimchukia ndugu yake sana na alipanga kumuua.

Rebeka alijua kwamba Esau alimchukia Yakobo na alipanga kumuua. Aliamua kumtorosha Yakobo mpaka Esau apunguze hasira yake. Isaka na Rebeka waliambia Yakobo, “Kwa heri,” na akaondoka kwenda safari ndefu ya Harani kwa mjombake Labani.

Yakobo alikaa Harani kwa miaka mingi. Alifanyia mjombake kazi. Yakobo alioa alipokuwa Harani na akapata watoto wengi. Baada ya muda mrefu alirudi kuishi nyumbani kwao nchi ya Isreali.